

TAARIFA KWA UMMA

WITO WA KUPATA MAONI KUHUSU OMBI LA KUREKEBISHA BEI LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA YA MUSOMA (MUWASA).

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imepokea ombi Na. **TR-W-09-010** kutoka **MUWASA** ya kurekebisha bei ya huduma inazozitoa. Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, EWURA inaanzisha mchakato wa kupata maoni ya wadau ili kujua uhalali wa ombi ililolipokea.

Katika mchakato huo, EWURA itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, wakiwamo Baraza la Wawakilishi wa Watumiaji wa huduma (CCC); Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) pamoja na wananchi. Mkutano wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau utakafanyika kwenye **Ukumbi wa Musoma Club (MUSOMA), Alhamisi, tarehe 29 Oktoba 2009 kuanzia saa nne (4) asubuhi**. Wadau wanaopenda kutoa maoni yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA ndani ya kipindi cha wiki mbili baada ya mkutano huo.

Wadau watakaopenda kuweka pingamizi kwenye ombi hili wanatakiwa kuonyesha nia yao kwa kuiandikia EWURA ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya tangazo hili. Wadau wote watakaoweka pingamizi watapata muda kuwasilisha maoni yao katika mkutano huo na pia watakuwa na fursa ya kupata nyaraka zote zilizowasilishwa na Mwombaji kwa kulipia gharama kidogo za kudurufu nyaraka hizo.

Nakala ya maombi na nyaraka za **MUWASA** zilizowasilishwa EWURA zinaweza kusomwa na mtu yeyote wakati wa saa za kazi kati ya saa 3 asubuhi na saa 11 jioni katika ofisi za EWURA. Wadau wanaombwa kuzingatia muda uliopangwa ili kufanikisha zoezi hili.

Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kuiandikia EWURA kwa anuani iliyotajwa hapo juu.